

Sominee Burungaisoo!

Tusome Kiburunge!



Kitabu cha msingi kwa wasomaji wa awali

Lugha ya Kiburunge



Cocoanee
Burungaisoo

Sominee Burungaisoo!

Tusome Kiburunge!

Kitabu cha Awali kwa Kiburunge ambacho kitatumiwa na
mwanafunzi au mwanafunzi pamoja na mwalimu.

Waandishi: Timu ya SIL.

Ushauri kutoka kwa **Samson Joseph Biira & Magdalena Jackson**
Michoro imechorwa na Adamu Peter Biira, Abdilatifu Salumu
Dengu, Kasimila Gabrieli, Mch. Amos Elias Jumbe, Thomas K.
Nahhadoo, Wilson Saki, Adamu Bakari Saidi na Liz Thomson.

Michoro mingine imetoka *International Illustrations*
CD © 2001 SIL International Literacy Department

Hadithi za Mila na Desturi zimeandikwa na Mch. Amos
Elias Jumbe na Salome Boo/a.

Toleo la Nne

Jinsi ya kutumia kitabu hiki

Kitabu hiki kimeandikwa mahsus i ya ajili ya Waburunge wanaopenda kujifunza jinsi ya kusoma na kuandika lugha yao. Mtu ye yote ambaye aliyejifunza jinsi ya kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili, anaweza kuki tumia kitabu hiki na baada ya kupata masomo machache pia atawezu kujua jinsi ya kusoma na kuandika Kiburunge.

Kitabu hiki kina masomo 17. Kila somo limeanza na maelezo mafupi juu ya herufi fulani. Baada ya maelezo hayo kuna mifano ya Kiburunge yenyeye herufi hizo. Ukihindwa kusoma maneno hayo, kuna tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili ili kukusaidia kugundua maana yake. Baada ya kuzoea kusoma maneno hayo kwa Kiburunge kuna nafasi zilizoachwa wazi zenye mistari kwenye kila somo, ili uweze kufanya mazoezi ya kuandika Kiburunge. Usiwe na wasiwasi kuandika kwenye kitabu hiki, kimetengenezwa kwa kazi hii! Ni daftari lako!

Mwishoni mwa kitabu hiki kuna majibu ya mazoezi yote. Baada ya kufanya zoezi la somo fulani unaweza kuangalia hapo na kusahihisha kazi yako. Usiangalie kabla ya kumaliza mazoezi yako. Ukiangalia mapema hutajifunza chochote.

Kuna kitabu kingine ambacho kitakusaidia kujifunza zaidi kuhusu jinsi ya kuandika Kiburunge. Kitabu hicho kinaitwa, “Guyaadimiisay gu Handikiru gu Burungaisoo” au (“Mwongozo wa Mwandishi wa Kiburunge”) Ukitaka nakala ya kitabu hicho, uwasiliane na Ofisi ya SIL huduma ya lugha Goima, Kondoa, na Dodoma anwani yetu imeandikwa hapo chini.

Shukrani

Tunataka kutoa shukrani kwa hawa watu ambao walitusaidia kutayarisha na kutunga kitabu hiki, hasa **Samson Joseph Biira na Magdalena Jackson** ambao walisahihisha muswada wa kitabu hiki. Tunawashukuru kwa mapendekezo na ushauri wao mzuri.

Maoni au mapendekezo yako


Ukikuta kosa lolote ndani ya kitabu hiki, au ukiwa na swali au pendekezo lolote au ukihitaji nakala nyingine ya kitabu hiki, naomba uwasiliane na:

Anna Saini, Ofisi ya Huduma ya Lugha ya Kiburunge Goima Anwani ya Posta: S.L.P. 97, SIL, Kondoa.

Au Ofisi ya Lugha, Kondoa mjini, karibu na Choka Gesti.

Somo la 1

Ulishajifunza jinsi ya kusoma na kuandika Kiswahili. Sasa ukipenda kujifunza Kiburunge kutachukua masaa machache tu! Hapo chini kuna maneno ya Kiburunge ambayo tayari unaweza kuyasoma. Herufi zifuatazo umeshajifunza tayari, kwa mfano: **a, b, d, g, i, m, n, r, s, u**



mara

Kiburunge

mara

saga

daba

dinu

mibi

dagara

amasi

Kiswahili

nyumba

kichwa

mkono

asali

kumi

mguu

usiku

Jaribu zoezi lifuatelo. Andika neno la Kiburunge kwa kila neno la Kiswahili. Herufi ya kwanza ya kila neno la Kiburunge imeshaandikwa:


asali	<u>dinu</u>
kumi	<u>m</u>
kichwa	<u>s</u>
nyumba	<u>m</u>
mguu	<u>d</u>
mwali	<u>d</u>
habari	<u>g</u>
mimi	<u>a</u>
jina	<u>u</u>
mtungi	<u>s</u>

Hongera! Umeshaanza kuandika Kiburunge! Endelea na masomo yafuatayo na utafafulu kabisa kusoma na kuandika Kiburunge.

(Unaweza kutumia “Gyaadimiisay gu Handikiru gu Burungaisoo,” yaani “Mwongozo wa Mwandishi wa Kiburunge,” kama msaidizi wako. Kuna maelezo zaidi kuhusu lugha yako kwenye kitabu hicho.)

Somo la 2

Sasa tuongeze herufi zaidi ambazo unazijua: **e, f, h, j, k, l, o, p, t, w, y.**



Fala

Kiburunge

fala

hotu

tami

yondu

kebabu

kori

tipa

bonda

yede yade

waka

jumati

Kiswahili

ngozi

mtoto wa kike

tatu

kazi

mafiga

mwaka

udongo (mchanga)

shimo

kule

nyingine

wiki hii

Fanya zoezi la kujaza maneno hapo chini:

- | | | |
|-----|---------------------|---------|
| 1. | mafiga | k _____ |
| 2. | jogoo | k _____ |
| 3. | nyumba | m _____ |
| 4. | shimo | b _____ |
| 5. | usolo | t _____ |
| 6. | ngozi | _____ |
| 7. | mototo wa kike | _____ |
| 8. | Mwingine (mwanamke) | w _____ |
| 9. | mtungi | _____ |
| 10. | mguu | d _____ |
| 11. | kazi | y _____ |
| 12. | tatu | _____ |

Somo la 3

Tena kuna herufi zingine katika Kiswahili ambazo umeshazizoea, yaani: **gw**, **kw**, **kh**, **ny**, **ch**. Ingawa herufi hizo zinaandikwa kwa herufi mbili, zinawakilisha sauti moja tu. Sauti **ch** hutokea mara chache katika Kiburunge na kwa kawaida inatumika kwa maneno yaliyokopwa kutoka kwenye Kiswahili, k.m. **chupaa**. Sauti **kh** inatokea kwa nadra sana katika Kiswahili, lakini inatumika sana katika Kiburunge. Pamoja na herufi **kh** kuna sauti nyingine katika Kiburunge ambayo inawakilishwa na **khw**. Herufi hii haipo katika Kiswahili lakini inatokea mara nyingi katika Kiburunge.

Soma maneno yafuatayo yenyе herufi hizo:



gwereti

Kiburunge

gwereti

khapu

yakway

nyeraw

chupaa

khwayla

sakhuru

Kiswahili

mbuzi dume

kosho

ng'ombe

nge

chupa

mtoto wa kike

kutwanga

Fanya zoezi lifuatalo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi:

kosho	<u>kh</u> apu
mtoto wa kike	<u>mt</u> ot <u>o</u> <u>w</u> a <u>k</u> ike
ng'ombe	<u>ng'</u> ombe
mbuzi dume	<u>mb</u> uzi <u>d</u> ume
chupa	<u>ch</u> upa
kusikiliza	<u>ku</u> si <u>kili</u> za
nge	<u>n</u> ge

Somo la 4

Kuna sauti zingine katika Kiswahili ambazo huandikwa tofauti katika Kiburunge. Katika Kiswahili kuna sauti **ai**, **ei**, **oi** na **ao**, k.m. **chai**, **bei**, koroboi na ubao. Katika Kiburunge kuna sauti zinazofanana kiasi na hizo za Kiswahili lakini zinaandikwa tofauti, yaani **ay**, **ey**, **oy**, na **aw**. Angalia maneno yafuatayo yalivyoandikwa:



Lagabay

Kiburunge

lagabay

makay

tigay

yakway

oday

pumbujay

pasliyey

Qoriidiyey

goy

aw

daw

nyeraw

Kiswahili

chungu cha kulia mboga

wanyama wa porini

wanawake

ng'ombe

udo

nyuki dume (wengi)

siyo wenyewe

hawana chakula

yangu

ng'ombe dume

tembo

nge

Jaribu zoezi lifuatelo. Andika neno la Kiburunge kwa kila neno la Kiswahili:

wanawake tigay

yangu g

ng'ombe dume a

anga r

wanyama wa porini m

mtoto wa kiume n

ninyi u

nge ny

Siyo wenyewe p

Somo la 5

Kiswahili kina irabu (vokali) 5, lakini Kiburunge kina irabu 15.


Kiburunge kinatofautisha irabu fupi, irabu ndefu na irabu zenyenye pumzi inayopitia puan. Kwenye somo hili tutajifunza jinsi ya kuandika irabu ndefu na kuzitofautisha na irabu fupi.

Irabu fupi: **a, e, i, o, u**

Irabu ndefu: **aa, ee, ii, oo, uu**

aă, eĕ, iĩ, oõ, uũ

Soma maneno yafuatayo jinsi yalivyoandikwa. Unapoyatamka jaribu kusikiliza tofauti kati ya maneno yenye irabu fupi na yale yenye irabu ndefu:



<u>Kiburunge</u>	<u>Kiswahili</u>	<u>Kiburunge</u>	<u>Kiswahili</u>
ila	jicho	aaraa	mbuzi
ilaa	macho	afa	mdomo
eaă	masikio	hadee	mwanamke
eeă	sikio	yede/yade	kule
ina	yeye	uurii	panzi

iinaa	deni	kori	mwaka
obu	mininga (aina)	kooloo	jembe
oonu	kibuyu (aina)	bosoroo	uwele
urunga	pua	magiiduu	kuni
uuriya	nyonga	yondu	kazi

Fanya mazoezi kwa kuandika irabu fupi na irabu ndefu kwenye maneno yafuatayo:

jina	<u>uma</u>	macho ____l____
popo	k__r__k__r__	sikio _____
mojamoja	l__l__l__l__	nyoka d__s__
mwaka	k__r__	panzi__r__
uwele	b__s__r__	jembe k__l__

Sasa kuna mazingira fulani ambapo tunaandika irabu fupi tu, ingawa matamshi yake ni ndefu. Angalia maneno yafuatayo. Utagundua kwamba ndani ya maneno hayo kuna m au n (sauti hiyo huitwa ‘nazali’) halafu konsonanti nyingine, **km.** **mp**, **mf**, **nd**, **nch**, **nk**, **ns**, **nt**. Irabu zinazotangulia na sauti hizo (yaani konsonanti zinazotanguliwa na nazali) hutamkwa ndefu kila mara. Kwa sababu hiyo siyo lazima kuziandika ndefu kwa sababu kila Mburunge atajua tu kwamba kabla ya sauti hizo irabu zitamkwe ndefu.*

<u>Kiburunge</u>	<u>Kiswahili</u>	
gompay	mwamba	(siyo: goompay)
gamfa	kidevu	(siyo: gaamfa)
danda	mgongo	(siyo: daanda)
munchere	wali	(siyo: muunchere)

inkoo	sasa	(siyo: iinkoo)
lensee	hata moja	(siyo: leensee)
aansaa	hadithi	(siyo: aansaa)
tantiru	kusonga ugali	(siyo: taantiru)

(*Angalia "Mwongozo wa Mwandishi wa Kiburunge" uk.8)

Fanya zoezi hili kwa kuandika irabu fupi na irabu ndefu kwenye maneno yafuatayo:

mgongo	d <u>a</u> n <u>d</u> a
uso	p <u> </u> n <u>d</u> <u> </u>
sasa	<u> </u> n <u>k</u> <u> </u>
mdomo	<u> </u> f <u> </u>
kidevu	g <u> </u> m <u>f</u> <u> </u>
wali	m <u> </u> n <u>ch</u> <u> </u> r <u> </u>
lete!	h <u> </u> n <u>d</u> <u> </u> !
mtu	h <u> </u> d <u> </u>
yeye	<u> </u> n <u> </u>
ngumi	k <u> </u> n <u>d</u> <u> </u>
pimbi	k <u> </u> n <u> </u>
mjomba	m <u> </u> m <u> </u> y
mafua	t <u> </u> mb <u> </u>
nge	ny <u> </u> r <u> </u> w
kijiji, mtaa fulani	t <u> </u> ng <u> </u>
kazi	y <u> </u> n <u>d</u> <u> </u>
nchi	y <u> </u> m <u> </u>
habari, shida	g <u> </u> mb <u> </u>
nguruwe pori	b <u> </u> n <u> </u>
magunzi	b <u> </u> ng <u> </u> y

Somo la 6

Kiburunge kina aina nyingine za irabu, yaani irabu zenyen pumzi inayopitia puan. Tunaandika irabu hizo kama ifuatavyo: **aā, eē, iī, oō, uū**

Alama ya kistari kilicho jikunja inaitwa ‘tilde’. Tunaitumia kwa kutofautisha irabu zenyen pumzi inayopitia puan na irabu fupi au ndefu. Alama hiyo iandikwe juu ya herufi ya pili, yaani **aā**, siyo **āā**, **a~a** wala **aa**.

Irabu zenyen pumzi inayopitia puan hutoke **mwishoni mwa maneno tu!** Hazitokei mwanzoni wala katikati ya maneno (ila kwa neno **oō**, kwa sababu halina herufi nyingine. Pia kwa neno, **ihiī'i**, imeamuliwa kuwa na tilde katikati, lakini ni kwa neno hilo tu).

Soma maneno yafuatayo yenyen irabu zenyen pumzi inayopitia puan:



baruū

<u>Kiburunge</u>	<u>Kiswahili</u>
baruū	mtama
madeē	masika
kataā	nundu
kibiriī	shina
oō	mlima

Sasa fanya zoezi hili, jinsi ya kuandika tilde juu ya herufi. Kwanza rudia kuandika herufi ambazo zimeshaandikwa kwenye rangi ya kijivu, halafu andika kwenye mistari bila msaada:

aā	aā	andika mara nne zaidi:	_____	_____	_____	_____
eē	eē	andika mara nne zaidi:	_____	_____	_____	_____
iī	iī	andika mara nne zaidi:	_____	_____	_____	_____
oō	oō	andika mara nne zaidi:	_____	_____	_____	_____
uū	uū	andika mara nne zaidi:	_____	_____	_____	_____


Jaribu zoezi lifuatalo. Andika neno la Kiburunge kwa kila neno la Kiswahili:

shina	<u>kibiriī</u>
nundu	<u>k</u>
mshale	<u>f</u>
watu wote	<u>hida g</u>
kiti	<u>k</u>
moja	<u>l</u>
masika	<u>m</u>
mlima	<u></u>
nyuma	<u>a</u>
kiuno	<u>kh</u>

Somo la 7

Kuna herufi za Kiburunge ambazo hazipo kabisa katika Kiswahili. Mojawapo ni c. Maandishi yake yanafanana kiasi fulani na **ch**, hata matamshi yake yanafanana, lakini ni sauti tofauti, kwa hiyo iandikwe tofauti.

Soma maneno yafuatayo:



catay

<u>Kiburunge</u>	<u>Kiswahili</u>
catay	kisu
cada	mbili
khoca	njoo!
cufa	jasho
ceedee	damu
ciimaa	chatu
colokhondiya	gamba la konokono
dabacu	mchuzi

Fanya zoezi lifuatalo. Andika neno la Kiburunge kwa kila
neno la Kiswahili:

mbili cada

twiga _____

kidole _____

kifuko cha nyongo _____

ulimi _____

ncha, kilele _____

ukucha _____

Somo la 8

Herufi nyingine ambayo ipo katika Kiburunge lakini haipo katika Kiswahili ni **hh**. Ingawa sauti hiyo inawakilishwa na herufi mbili, ni sauti moja.

Soma maneno yafuatayo:



hhadaa

<u>Kiburunge</u>	<u>Kiswahili</u>
hhadaa	fimbo
hhoora	minyaa
hhurii	ndege (aina)
cigahha	nne
hherehheraa	machozi
hhinihhinii	maboga
kwahhasi	karibu!

Malizia sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno ambayo
yameandikwa chini:

1 . Hiĩ na catay gu _____

2 . Haa yaamu haloo _____ ?

3 . La _____ ayage.

4 . Ana haã _____ kweerage.

5 . Yaa _____ dahhi.

6 Yaani _____ cheeti.

dahhada hhiyuma leehhisi

dihhu hhamaahhami cehheemisida

Somo la 9

Herufi **q** katika Kiburunge haipo kwenye Kiswahili. Ipo kwenye Kiingereza lakini sauti yake ni tofauti.

Soma maneno yafuatayo:



qaymoo

Kiburunge

qaymoo

quubu

qeeraa

qipaa

qori

caqaru

daqa

teqeesay

Kiswahili

shamba

nywele

uwerevu

mayai ya chawa

njaa

mapambo

sehemu, eneo

hivi

Angalia jinsi **q** ilivyoandikwa: kichwa chake kinagusa mstari na mguu wake unaelekea chini. Uwe mwangalifu unapoiandika kutofautisha **q** na **g** na namba **9** na p.

Fanya mazoezi jinsi ya kuiandika. Kwanza rudia kuandika herufi ambayo imeshaandikwa kwenye rangi ya kijivu, halafu andika kwenye mistari bila msaada:

q q andika mara nne zaidi: _____

Herufi yake kubwa ni Q . Inabidi ujifunze jinsi ya kuandika herufi hii. Uwe makini kutofautisha herufi hiyo, Q, na herufi kubwa ya irabu O. Herufi Q ina mkia mfupi.

Fanya mazoezi jinsi ya kuiandika herufi kubwa:

Q Q andika mara nne zaidi: _____

Kuna herufi nyingine inayofanana na q ambayo ni qw (herufi kubwa yake ni Qw).

Soma maneno yafuatayo:



qwaaama

Kiburunge

qwaaama

qweelii

caaqwaa

qwiliqwincoo

daqway

Qwancaee

Kiswahili

zizi la ng'ombe

mzizi (kama vitunguu)

baridi

viasi vitamu vidogovidogo

punda

Wagogo

Fanya mazoezi kuhusu **q** na **qw** kwa kujaza maneno yafuatayo
katika fumbo linalopatikana hapo chini:

1. Wagogo -----
2. Shuka -----
3. Mate -----
4. Punda -----
5. Njaa -----
6. Kusubiria -----
7. Eneo -----
8. Uwerevu -----
9. Mzizi (kama vitunguu) -----
10. Saba -----
11. Tamu -----

Somo la 10

Herufi tl hutumika katika Kiburunge lakini haipo katika Kiswahili. Sauti hiyo inatokea mara nyingi katika Kiburunge. Soma maneno yafuatayo:



tlubay

Kiburunge

tlubay

tleemaa

tlonga

tlawa

tlitliqisi

qatlay

dantla

Iiitleemu

Kiswahili

mvua

mchana, juu

mawingu

ziwa

gundisha!

wakati

mnana

Mungu

Jaribu zoezi lifuatalo. Andika neno la Kiburunge kwa kila neno la Kiswahili:

asubuhi heetlawaa

Kesho _____

mtetemeko wa ardhi _____

mawingu ya mvua _____

Mwanzo _____

mtego wa kanga au kware _____

Njiwa _____

Uji _____

fundi (wa kujenga nyumba) _____

wivu _____

ndoto _____

Somo la 11

Herufi **sI** hutumika katika Kiburunge lakini haipo katika Kiswahili. Mara nyingi watu wanapata shida kuisoma na kuiandika herufi hiyo. Kwa hiyo soma maneno yafuatayo na jaribu kukumbuka jinsi yanavyoandikwa.



slee

Kiburunge

slee

slabaslaba

slubisay

slifoo

slonkheenaa

aslaa

khisla

dooslimiisay

Kiswahili

ng'ombe (jike)

mchwa

pekecho

midomo

pango la pua

moto

sana

Jaribu zoezi lifuatalo. Andika neno la Kiburunge kwa kila
neno la Kiswahili:

mwili

slaqwa

Majani

vitu, vyombo

Mchawi

kumbe!

Kinyonga

Mwezi

Uji umepikwa. Tlaatlaqwaa dagaā

Wamekutana Hangii

Somo la 12

Kuna sauti maalum katika Kiburunge ambayo haipo katika Kiswahili. Kwenye alfabeti ya Kiburunge tunatumia alama hii / (mkwaju) kwa kuwakilisha sauti hiyo. Herufi / haina alama maalum kwa kuonyesha herufi kubwa. Kwa hiyo alama hiyohiyo, yaani / inatumika kama herufi ndogo na herufi kubwa pia.

Soma maneno yafuatayo:



/aslaw

Kiburunge

/aslaw

/oona

fa/a

/embee

/ura

/insoolay

du/iyā

go/onay

bee/u

kwa/ii

Kiswahili

mnangari

giza nene

ugali

uchafu (katika chombo

chochote au kisimani)

majivu

mshale wenyе rungu kichwani

mafuta

vibuyu (aina)

kondoo

sungura

Ukiandika kwa mkono, uwe mwāngalifu kutofautisha / na l
vizuri, ili usichanganye herufi hiso.

Malizia sentensi hizi kwa kutumia maneno ambayo yameandikwa
hapo chini:

1. Hiī _____ tuku!

2. Tlehhidiisay hiī _____ mara goy.

3. Gumaa _____ kaw letu wakay.

4. Sinaa qayde catay gu _____

5. Haguū _____ slabaslabā goō.

6. Diidaw dugu _____ ha hida

boo/imisi

coko/u

ba/aa/ati

wa/a

ciri/idaa

gwaa/i

cu/i

Somo la 13

Herufi ' (mkato wa juu) inawakilisha sauti inayotamkwa kwa kuibana hewa ghafla katika koo na kuiachia tena ghafla. Sauti hiyo haipo katika Kiswahili. Katika Kiburunge huandikwa tu ikijitokeza katikati ya irabu mbili sawasawa. Soma maneno yafuatayo:



ba'ara

Kiburunge

ba'ara

ma'ay

embere'ee

ii'imoo

coco'omoo

fu'umay

bu'uu'uru

Kiswahili

nyuki

maji

viwavi jeshi

nyoka (aina)

maongezi

nyama

wakati wa mavuno

Uwe mwangalifu kutofautisha irabu ndefu, k.m. **aa, ee, ii, oo, uu**, na irabu ambazo zina mapumziko kidogo katikati, yaani **a'a, e'e, i'i, o'o, u'u**.

Kufuatana na kanuni za Kiburunge hatuhitaji kuweka mkato wa juu ['] katikati ya irabu tofauti tofauti kwa sababu kila Mburunge anaposoma atajua tu kutamka na mapumziko katikati ya irabu hizo. Kwa hiyo tuandike **tiaa**, siyo ti'aa; **kooani**, siyo koo'ani; **Burungaisoo**, siyo Burunga'isoo.

Herufi ' inaandikwa katikati ya irabu sawasawa tu. Lakini siyo lazima uandike mkato wa juu kila mahali unapokuta irabu sawasawa kwa sababu inawezekana kwamba irabu hizo zinawakilisha irabu ndefu, k.m. **aaraa** (mbuzi), kuna irabu ndefu mwanzoni na mwishoni, usiandike **a'ara'a!**

Fanya zoezi lifuatalo ili ujifunze wapi inabidi kuweka mkato wa juu.
Kuna maneno yenyе mkato wa juu na kuna maneno ambayo hayana.
Maneno yote yameandikwa bila mkato wa juu. Kazi yako ni
kuyaandika tena na kuweka mkato wa juu kama ni lazima. Kama sio
lazima rudia kuandika tena kama ilivyoandikwa. Kuna mifano miwili
inayokuonyesha taratibu hiyo:

maji	maay	<u>ma'ay</u>
kutoka hapa	tiaa	<u>tiaa</u>
nyama	fuumay	_____
wakati wa mavuno	buuuuru	_____
tano	kooani	_____
mbuzi	aaraa	_____
hapo kwako	teesii	_____
Mburunge (mwanamke)	Burungitooo	_____
Kiburunge	Burungaisoo	_____
moyo	muuna	_____
chui	duuma	_____
kwa nini?	sooy	_____

Somo la 14

Lugha nyingi zinatofautisha maana kwa kutamka vokali (irabu) kwa sauti tofauti tofauti. Hata Kiburunge kinatumia sauti ya juu na sauti ya chini katika irabu fulani. Sauti hizo zinaitwa *toni*.

Inabidi tuandike tofauti moja tu: tukimaanisha *wakati utakaokuja* tuandike [oo], tukimaanisha *mazoea* fulani tuandike [oo]. [oo] inatamkwa bila sauti kushuka wala kupanda, [oo] inatamkwa kwa sauti inayopanda.

k.m.:

Yoo khufi. Atakunywa (pombe). (wakati utakaokuja)

Yoó khufi. hunywa (pombe). (mazoea)

Yoo hha'aluumidiyyay. Watafurahi. (wakati utakaokuja)

Yoó hha'aluumidiyyay. hufurahi siku zote. (mazoea)

Alama ya toni, yaani ‚, hujitokeza kwenye oo tu, haipo kwenye herufi nyingine. Pia iandikwe juu ya o ya pili, yaani oo, siyo oo wala oo.

Sasa umeshajifunza alama mbalimbali ambazo ni ndogo na zinazokaa juu au katikati ya herufi nyingine. Ni muhimu sana kutofautisha alama hizo: oo, oõ, o'o, na oó. Soma maneno yafuatayo:

<u>Kiburunge</u>	<u>Kiswahili</u>
oo	chukua!
oõ	mlima
coco'omoo	maongezi
Yoo khufi	Atakunywa.
Yoó khufi	Hunywa.

Mazoezi

Tafsiri sentensi zifuatazo kutoka katika Kiswahili kwenda kwenye Kiburunge:

1. Khankhay atakuja. **Khankhay yoo khay.**

2. Huwa nalima. **Hoó doosla.**

3. /awtu huniangalia. _____

4. Soolay atanyonya. _____

5. Khankhay huwa anakuja. _____

6. Nitachunga. _____

7. Nitalima. _____

8. Soolay hunyonya. _____

9. Mimi huwa nachunga. _____

10. /awtu ataniangalia. _____

Somo la 15

Sasa umejifunza kila kitu ambacho kinahitajika ili uweze kusoma Kiburunge. Sasa hivi kuna nafasi ya kufanya mazoezi ya kusoma. Soma hadithi zifuatazo:

Kwa/ii haa Slangaslangay

“Ansaa!”

“Haaya, haaya!”



Yaa wanta baloo waka Kwa/ii haa

Slangaslangay hingaa slaslayri amooge, hingigi tooinaa cehheemisiri. Haa Slangaslangay bee, “Hiiye, ya'a koku gu so'oy cohhi taqay dee gu lou, ugu hoóy dahhamisidaa tu/udimoo?”

Kwa/ii gi ilaki/isi, ina bee, “Ugu haa bawti.” Hikira bee, “Hiiye, sa so'oy teqeesay kaada, poo bere ma tlaatleesani tu/udimoo, sa heedi doo kaba/eye.” Teesaa kwa/ii gi tosaa slahhaai, ina bee, “Nara'a.”

Tooinaa qadimidiri, ginaa ilii tlaatleesiri tu/udimoo. Slangaslangay daa cirihhi goo, gi tosaa gii tlo/osi danda gu Kwa/iige. Kwa/ii tosaa ilaqinci tu/udimoo, Slangaslangay kogo/o dandage.

Qatlay giyaa ilii dayri daqatiray hingaa ilii ila/imbidirige, Slangaslangay yaatii tlo/osi, “Jika/a!” pandaage, gi tosaa kaay, ina bee, “Haā antii ana gungii cati. Ugu hhidinta tu/udimoo.” Kwa/ii dugwaa teesaaqay hiidahhasi ha Slangaslangay. Ti'ii na nambaranamboo dosi.


Iinaa gu Nyaa uu haa Ungusimoo

Letu waka nyaa uu yaa konta slaqumu qaymoo dosii. Higi tosaa waauti kakaruuge sa ungu su, kaslenkwa a nyaa uu hitii nahaahata ungu su sa /agoo dooina.

Giyaa ilii daadi maraai gu ungu suge sagaati kaay tuba, “Ee nara'a, da pisiye hoo khayna heetlaalee.”

Daa ilii pisi, nyaa'uu goō yaay ca/iri qaymoo da nyaa uu dono'oo dooinay, tooinaa tlaatleesiri doosla te'esii. Ungusu see naa bawma dosi yaagi tosaa khay slaqumuge, yaati tafai hari amoo leē. Kaslenkwa a, nyaa'uu cada hiī nahhamidiri amooge, gitii guniri qaymooge digaati ba/i alungo ha wakinay. Ungusu yaati bakaakai. Te'esaa nyaa'uu gi tooinaa tlaatleesiri coco'omoo tuba, “Inkoo hiiqonee, leē ungu simoo, leē ungu simoo.” Ungusu, kaslenkwa a, hiī bonderiige qadimidi, te'esaa na “Hururuku!” bondeeriige. Nyaa'uu yaa /aa/iri te'esii, ungu su diī wa'ayge.

Letuti see ungu su inaa nyaa uu nangooti wakaawakiyay letuti naqatloo.



Somo la 16

Baada ya kujifunza machache mengine utapata nafasi kuandika hadithi yako wewe mwenyewe.

Kwenye maandishi ya lugha yoyote ni muhimu kujua mipaka ya maneno na kuweka nafasi katikati ya maneno ili kumsaidia msomaji kujua neno moja linaishia wapi na neno lingine linaanza wapi. Bila nafasi katikati siyo rahisi kusoma. Angalia sentensi zifuatazo ambazo hazina mipaka wala nafasi katikati ya maneno:

*Yaawantabaloowakakwa/iihaaSlangaslangayhingigislaslayri
amoogeHingigicehheemisirihaaSlangaslangay.*

Ni vigumu kusoma, sivyo?

Mara nyingi mipaka katikati ya maneno itagunduliwa tu bila kuifikiria sana. Mwandishi akijisomea maandiko yake polepole, atagundua mapumziko kidogo katikati ya maneno. Mara nyingine ni vigumu kugundua mipaka hiyo. Hapo chini kuna maamuzi machache yanayohusu jinsi ya kutenga maneno mengine katika Kiburunge.

Vionyeshi

Maneno ambayo yanaonyesha kitu fulani kiko mahali fulani, kulingana na mahali alipo msemaji, yanaitwa *vionyeshi*. Kwa

Kiburunge kuna vionyeshi vifuatavyo (*angalia herufi nzito tu*):

micookoo	panda ^a	ilibaa
micoookoki	pandati	ilibaa hhanki
micoookokee	pandatee	ilibaa hhakee
micoookoka'a	pandata'a	ilibaa hhaka'a
micoookokira	pandatira	ilibaa hhakira

Kwenye kanuni ya Kiburunge vionyeshi **-ki**, **-kee**, **-ka'a**, **-kira**, **-ti**, **-tee**, **-ta'a**, na **-tira** viunganishwe na nomino zao, k.m. **micoookoki** na **pandatee**, na vionyeshi **hhanki**, **hhakee**, **hhaka'a** au **hhakira** vitengwe na nomino yao, k.m. **ilibaa hhanki**.

Mazoezi

Angalia maneno yafuatayo na uthibitishe kama yameandikwa sawa au si sawa. Kama ni sawa weka y kwenye boksi, kama si sawa weka X kwenye boksi na andika tena kama inavyotakiwa kuandikwa. Angalia mifano miwili mwanzoni, halafu uendelee vivyohivyo na maneno mengine:

Ni sawa au si sawa?

**Isipokuwa sawa andika kama
inavyotakiwa**

micookookee

x

micookookee

ilibaa hhakira

Pandatira

yakwayhhakee

hadee ti

sagaka'a

mara kira

daqa tiray

heedikee

aaraa hhanki

Vimilikishi

Maneno yanayoonyesha uhusiano wa kitu fulani kuwa mali ya mtu fulani huitwa *vimilikishi*. Katika Kiburunge kuna vimilikishi vifuatavyo (angalia herufi nzito tu):

dahaa goy	kuugiya doy	ilibaa koi
dahaa googu	kuugiya doogu	ilibaa koku
dahaa googi	kuugiya doogi	ilibaa koki
dahaa gosi	kuugiya dosi	ilibaa kosi
dahaa goori	kuugiya doori	ilibaa koti
dahaa googuna	kuugiya dooguna	ilibaa kokuna
dahaa gooina	kuugiya dooina	ilibaa koina

Vimilikishi vyote vitengwe na nomino zao.

Mazoezi

Tafsiri maneno yafuatayo kutoka katika Kiswahili kwenda kwenye Kiburunge:

mbuzi zetu	aaraa koti
kichwa changu	_____
mke wako	_____
mume wake	_____
shamba lenu	_____
maji yao	_____
kipekecho chake	_____
watoto wangu	_____

Somo la 17

Kitenzi ni neno ambalo linaleza tendo linalofanyika, k.m. qabe, handikimi, soidi. Kirai cha kitenzi ni fungo la maneno ambalo linaleza siyo tendo tu peke yake, lakini pia muda wake (zamani, sasa, kesho n.k.), mtendaji wake (mimi, wewe, yeze n.k.) na mambo mengine mengi.

Angalia sentensi ifuatayo:

Sa/alee **haā waaudi** wa/amuuge. (Jana nilikwenda kisimani.)

Kirai cha kitenzi kwenye sentensi hapo juu ni: **haā waaudi**. Kawaida katika Kiburunge, kila kirai cha kitenzi kina vipande viwili.

Angalia mifano ifuatayo:

Haā fici	nimefagia
Haa hhuncidi	ulioga
Yaa /aa/ii/imina	alikuwa analia
Hooy huu'uday	mtaanguka
Haguraani khayni	tumeshamleta
Lamaati tledayda	urefuke

Kwenye kanuni za Kiburunge vipande viwili hivyo viandikwe kwa kuvitenga, kwa sababu neno lingine linaweza kuingia katikati yao, k.m.:

Kumbo'oo yaa waauti. Mama mkwe aliondoka.

Kumbo'oo yaa ayago waauti. Mama mkwe aliondoka
kutoka nyumbani.

Kuna mfano mwingine ambao unatokea mara nyingi kwenye hadithi za Kiburunge. Angalia sentensi ifuatayo:

Kwa/ii ginaa ilii khay aya gu konkokuge ta, “Guutee, yeraa!”

Kwenye mfano huu neno **ilii linaingizwa** katikati ya vipande viwili vyatia kirai cha kitenzi. Kila sehemu itengwe, yaani iandikwe **ginaa ilii khay**, siyo **ginaailii khay**, wala **ginaa iliikhay**, wala **ginaailiikhay**.

Masharti hayo si rahisi kwa mwandishi kushika mara moja, kwa sababu mara nyingi kwenye matamshi yake ni kama neno moja tu, k.m. **haahhuncidi**. Pia inawakilisha dhana moja tu, na peke yake kipande hicho cha kwanza hakina maana bila kitenzi chenyewe (yaani kipande cha pili). Lakini ni muhimu kufuata kanuni za Kiburunge ili maandishi yako yalingane na Kiburunge sanifu.

Ili usaidiwe kuzoea jinsi ya kuandika kirai cha kitenzi, fanya mazoezi yafuatayo.

Kwenye sentensi zifuatazo zungushia kirai cha kitenzi. Angalia mifano miwili mwanzoni. Inawezekana kuwa na virai viwili vya vitenzi katika sentensi moja:

1. Sa/alee haā waaudi wa/amuuge.
2. Qatlay giyaa ilii day ayage, yaa huui.
3. Nyaa'uu yaa /aa/iri te'esii.
4. Neetoti haga sla'a.
5. Hootii laabana letu yaqa afa gu onke.
6. Diniī afahhami amoo.
7. Sini afioynte afamaraa!
8. Yaani hheekidii ma'ay?
9. Hingaa ilii slaslayri, ginaa ilii tlaatleesiri qwatla.
10. Hindaqaru yoó ibidiyaaba ina lee.
11. Tleemaa yaayii da/adi hari khisla.
12. Khaimoo goy dugoó iliidayaaaba.

Tafsiri sentensi zifuatazo kutoka katika Kiswahili kwenda kwenye Kiburunge:

1. Huyu mama atapika ugali.

Hadetee yoo tantinta fa/a.

2. Watoto walicheza vizuri.

3. Kesho tutakwenda mjini.

4. Alinipa gunia moja la mahindi.

5. Tulipofika kwao tulianza kusalimiana.

6. Umetosheka?

Sasa ni nafasi yako kuandika hadithi au historia fupi kwa Kiburunge. Labda unajua hadithi za wanyama, k.m. kuhusu **kwa/ii** au **baymoo** au **daw** au mnyama mwingine. Pengine unataka kuandika historia fupi kuhusu Waburunge au maisha yako. Pengine unataka kuandika kuhusu utamaduni au desturi ya Waburunge. Chagua hadithi yoyote unayoipenda! Tumia nafasi iliyopo hapo chini na kwenye karatasi zifuatazo kwa ajili ya kuandika hadithi au historia yako.

Hadithi yangu

Hadithi yangu

Majibu ya Mazoezi

Hii ni sehemu ya masahihisho. Linganisha majibu yako na majibu sahihi yafuatayo. Kama umekosea urudie tena somo hilo ili ujifunze vizuri jinsi ya kusoma na kuandika Kiburunge. Maneno mengine ya Kiburunge yanatamkwa kwa njia tofauti tofauti. Matamshi hayo yote ni sawa. Kwa hiyo kama umeandika neno fulani tofauti kwa ajili ya matamshi yako, hii siyo kosa, km. Somo la 5: kurukuruu, inawezekana kuandikwa kurukuroo.

Somo la 1

dinu, mibi, saga, mara, dagara, dagana, gimba, ana, uma, sibida

Somo la 2

1. kebabu, 2. konkaku 3. mara, 4. bonda, 5. tagadiya, 6. fala,
7. hotu, 8. waka, 9. sibida 10. dagara, 11. yondu, 12. tami

Somo la 3

khapu, khwayla, yakway, gwereti, chupaa, akhamisu, nyeraw

Somo la 4

tigay, goy, aw, raw, makay, naw, unkuray, nyeraw, pasliyey

Somo la 5

uma, ilaa, kurukuruu, eea, leleelelee, deesu, kori, uurii, bosoroo, kooloo, danda, pandaa, inkoo, afa, gamfa, munchere, hindo, heedi, ina, konday, kuuna, maamay, temba, nyeraw, tongoo, yondu, yaamu, gimba, biinoo, bingay

Somo la 6

kibiriĩ, kataã, fayuũ, hida goõ, kitii, leẽ, madeẽ, oõ, aluũ, khiriĩ

Somo la 7

cada, camasu, dinca, kwacankha, cufaraã, cina, carafu

Somo la 8

dihu, dahhada, cehheemisida, hhamaahhami, hhiyuma, leehhis.

Somo la 9

1. qwancae, 2.qayru, 3. cubuqari, 4. daqway, 5. qori, 6. baqamidu,
7. daqa, 8. qeeraa, 9. qweelii, 10. fanqu, 11. nuqu.

Somo la 10

heetlawaa, heetlaalee, kintla, tlafoo, tlaatleesoo, khotlombaa,
tlabiya, tlaatlaqwaa, tlehidiisay, tloomu, tletaa.

Somo la 11

slaqwa, sluufaa, khooslay, miisiislay, kaslenkwa, Slangaslangay,
slehheẽ, slubisi, slaslayri.

Somo la 12

ba/aa/ati, boo/imisi, ciri/idaa, coko/u, cu/i, gwaa/i, wa/a

Somo la 13

ma'ay, tiaa, fu'umay, bu'uu'uru, kooani, aaraa, te'esii,
Burungito'oo, Burungaisoo, muuna, du'uma, so'oy

Somo la 14 (Majibu ya Mazoezi)

Khankhay yoo khay, Hoó doosla, /awtu noó khu'una, Soolay yoo ru'unta, Khankhay yoó khakhay, Hoo de'ema, Hoo doosla, Soolay yoó ru'unta, Ana hoó de'ema, /awtu noo khu'una.

Somo la 16 **Ni sawa au** **Isipokuwa sawa, andika
kama inavyotakiwa kuandika.**

si sawa

Micookoo	x	<u>micookokee</u>
ilibaa hhakira	✓	_____
pandatira	✓	_____
yakwayhhakee	x	<u>yakway hhakee</u>
hadee ti	x	<u>hadeti</u>
sagaka'a	✓	_____
mara kira	x	<u>marakira</u>
daqa tiray	x	<u>daqatiray</u>
heedikee	✓	_____
aaraa hhanki	✓	_____

aaraa koti; saga goy; hadee doogu; hhawata gosi; qaymoo dooguna;
ma'ay koina; slubisay gosi; ya'ay koi (daaqay koi)

Somo la 17 (Majibu ya Mazoezi)

1. Sa/alee haā waaudi wa/amuuge.
2. Qatlay giyaa ilii day ayage, yaa huui.
3. Nyaa'uuu yaa /aa/iri te'esii.
4. Neetoti **haga** **sla'a**.

5. Hooti **laabana** letu yaqa afa gu onke.
6. Diniī afahhami amoo.
7. **Sina** **afioynte** afamaraa!
8. Yaani hheekidii ma'ay?

9. Hingaa ilii **slaslayri**, ginaa ilii tlaatleesiri qwatla.
10. Hindaqaru yoó ibidiyaaba ina leē.
11. Tleemaa yaayii da/adi hari khisla.
12. Khaimoo goy dugoó iliidayaaaba.

1. Hadetee yoo tantinta fa/a.
2. Daaqay (Ya'ay) yaa neetiniri hhoinay.
3. Heetlaalee dandiray hoo hoyomboo kayna.
4. Ina sinaa qay curuqu leē gu olongaa.
5. Qatlay gaa ilii daani yaamkoinay hangaa tlaatleesani
cehheehhemisu.
6. Haā bu'udisidii?

Shirika la SIL International limeenea katika maeneo mbalimbali, linahudumia lugha mbalimbali katika nchi zaidi ya 70 ulimwenguni kote. Zaidi ya mataifa 20 kati ya mataifa 70 yako Afrika.

Lengo la SIL ni kuinua utafiti wa kiisimu, maendeleo ya lugha, mafundisho ya kusoma na kuandika, tafsiri, pamoja na mambo ya kielimu na kutafiti utekelezaji wa huduma, kijamii na kimaendeleo.

Kwa upande wa mkoa wa Dodoma tunatoa huduma kwa makabila ya Waburunge, Warangi, Wasandawe na Waalagwa.

